**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 25 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.**

158. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kipindi cha karibuni nchi yetu imekumbwa na ongezeko la ajali za barabarani zinazotokana na kukiukwa kwa Sheria za Usalama Barabarani hasa kwa vijana ambao huendesha vyombo vya moto kwa kufukuzana na kusereреka na wengine kuinua juu vyombo vya moto vya maringi mawili na kwenda mwendo wa kasi wa hatari.

Je, Serikali kwa kushirikiana na jeshi la Polisi, kwanini wasiweke mkakati wa kudhibiti vijana hawa wanaofanya michezo hiyo ya hatari kwa kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria ili kukomesha michezo hiyo.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

212. MHESHIMIWA RUKIA OMAR RAMADHAN (Jimbo la Amani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi Rais, Fedha na Mipango:

Watu wenye ulemavu wana haki na wajibu sawa kama raia wengine. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sheria Nam. 9 ya watu wenye mahitaji maalum ya mwaka 2006 yenye lengo la kutunza fursa sawa kwa kuimarisha uwezeshaji, ushirika na kulinda haki za watu wenye mahitaji maalum, Sheria hiyo inasisitiza haja ya kuwa na mazingira rafiki katika majengo na miundombinu yote.

(a) Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilizindua muongozo wa Kitaifa wa viwango vya miundombinu rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum. Ni sababu zipi zilizopelekea kutotekelezwa kwa muongozo huo pamoja na kusimamia Sheria namba 9 ya mwaka 2006 kwa nia ya kutoa haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.

(b) Ni asilimia ngapi ya majengo ya umma yenye miundombinu rafiki yaliyojengwa kabla ya muongozo huo na asilimia ngapi yameongezeka baada ya muongozo huo.

(c) Kuna mpango gani wa kisheria ambao unalengo la kurekebisha majengo tuliyonayo sasa na yale yatakayopewa vibali vya ujenzi kuanzia mwaka huu ili yajengwe yakiwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

16. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa katika Mabaraza ya Miji ya Pemba mara nyingi tumeshuhudia magari pamoja na vyombo vyengine vya moto vikitozwa tozo la shilingi mia tano hadi shilingi elfu moja ya gharama za maegesho (parking fee), na kwa kuwa katika miji yetu hapa Pemba hakuna maeneo maalum ya maegesho ya magari ambapo wakati mwengine gari huegeshwa mahali pasipo na usalama.

(a) Je, ni lini Serikali itafikiria kujenga maegesho rasmi "parking" ya magari pamoja na vyombo vyengine vya moto katika miji ya Pemba.

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia pale linapotokezea tatizo kwa gari lililoegeshwa katika maegesho hayo.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

173. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kuna umuhimu mkubwa wa kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi iliyopangwa ili kuleta taswira sahihi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Je, ni taasisi gani rasmi inayohusika kufanya kazi hiyo kwa miradi inayotekelezwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

120. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Zipo taarifa za kupewa barua za kustaafishwa kazi kwa baadhi ya wagombea wa vyama mbali mbali vya siasa walioteuliwa kuwa wagombea katika vyama vyao, katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

(a) Je, ni Sheria ipi ambayo Mtumishi wa Umma aliyegombea nafasi ya kisiasa ya ubunge, uwakilishi na udiwani inayomzuia asirudi kazini baada ya kushindwa uchaguzi au kura za maoni katika Jimbo husika.

(b) Je ni utaratibu gani unaofuatwa kwa watumishi wa umma wanaotaka kugombea nafasi ya kiasa wakati wa Uchaguzi Mkuu au chaguzi mdogo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

66. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Kizimbani hadi Miwani imekuwa mbovu kwa muda mrefu sasa pamoja na kutajwa katika Ilani ya CCM kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, hadi sasa barabara hiyo haijajegwa na badala yake imekuwa inafanyiwa matengenezo madogo madogo kwa kutiwa kifusi. Barabara hiyi inaleta kero kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Kati na imekuwa ikizungumzwa katika bajeti ya kila mwaka na Serikali iliahidi kwamba barabara hiyo itajengwa mara tu baada ya kukamilika barabara ya Fuoni hadi Kombeni.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga barabara ya Kizimbani hadi Miwani kwa kiwango cha lami.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

179. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika Shehia ya Shamiani – Mwambe kuna Skuli ya Msingi ambayo ina banda moja linalosomewa ambalo ni bovu na halifai kwa wakati huu kuendelea kusomewa.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri umeshawahi kufanya ziara ya kuitembelea skuli hiyo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kulikarabati jengo la banda ya skuli hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

45. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Malisili na Mifugo:

Hivi karibuni baadhi ya shughuli za kilimo cha umwagiliaji zimegatuliwa katika Halmashauri za Wilaya, jambo ambalo pamoja na uzuri wa malengo yake, linaleta shida sana kwa wakulima, pia ni mzigo mzito katika Halmashauri zetu.

(a) Je, ni shughuli gani za umwagiliaji ambazo zinahamishiwa katika Halmashauri.

(b) Je, ugatuzi huu ulienda sambamba na vitendea kazi na wataalamu wa kilimo cha umwagiliaji.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**25 Mei, 2021.** **KATIBU WA BARAZA**